# SAUTI YA TSC

TOLEO NA.1 | JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC) | MACHI 2021

# NAIBU WAZIRI SILINDE AAGIZA TSC IPEWE OFISI ZENYE HADHI



*Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde akifungua Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), mjini Morogoro, Januari 25, 2021. Wengine kutoka kulia ni Mwenyekiti wa TSC Profesa Willy Komba, Kaimu Katibu wa TSC Moses Chitama na Katibu wa Baraza husika, Lawrence Chankani.*

**MAWASILIANO:** Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
**Simu:** +255 (26) 2322402-4 **Barua Pepe:** secretary@tsc.go.tz **Tovuti:** www.tsc.go.tz

*Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania* *tumeyautumishiwawalimutanzania*

# NAIBU WAZIRI SILINDE AAGIZA TSC IPEWE OFISI ZENYE HADHI



*Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde (kushoto), akisalimiana na Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Profesa Willy Komba, muda mfupi baada ya Naibu Waziri kufungua Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa TSC, mjini Morogoro, Januari 25, 2021. Katikati ni Kaimu Katibu wa TSC, Moses Chitama.*




*Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Profesa Willy Komba (kulia), akitoa hotuba ya ukaribisho wa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde (katikati), wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Tume hiyo, Januari 25, 2021 mjini Morogoro. Kushoto ni Kaimu Katibu wa TSC, Moses Chitama.*

**Na Veronica Simba**

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde amewaagiza Wakurugenzi wa Wilaya kote nchini, kuhakikisha wanawapatia ofisi zenye hadhi, watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) katika maeneo yao.

Alitoa maagizo hayo Januari 25, 2021 mjini Morogoro wakati akifungua Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Tume.

Naibu Waziri alitoa maagizo hayo baada ya kuelezwa changamoto mbalimbali zinazoikabili Tume husika, ambapo mojawapo ni ya ukosefu wa ofisi zenye hadhi kwa watumishi wa TSC hususani zilizoko katika baadhi ya Wilaya nchini.

"Nitumie fursa hii kuagiza Wakurugenzi wote nchini kuhakikisha wanawapatia Makatibu Wasaidizi wa Tume, ofisi ambazo zinaendana na hadhi ya utumishi wa umma."

> **“Sote tunafahamu kuwa tunapotoa huduma bora kwa Mwalimu inamwezesha kutekeleza majukumu yake shuleni kwa ufanisi hatimaye kuinua kiwango cha elimu nchini.”**

## NENO KUTOKA KWA KATIBU



**Moses Chitama**
***Kaimu Katibu TSC***

Ni ukweli ulio bayana kuwa kwa sasa Dunia imehamia katika mitandao. Kukua kwa teknolojia hususan katika sekta ya mawasiliano, kumezidi kurahisisha upashanaji habari na taarifa. Kupitia mitandao, taarifa na habari mbalimbali huweza kufikia idadi kubwa ya walengwa, tena ndani ya muda mfupi.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), imekuwa ikitumia mbinu mbalimbali za mawasiliano katika kuwafikishia wadau wetu, habari na taarifa zetu. Lengo letu ni kuufahamisha umma, kazi tunazozifanya kwa maslahi ya Taifa kwa ujumla wake.

Ni kwa muktadha huo, TSC imeona ni vyema kuanzisha Jarida hili la Mtandaoni, ikiwa ni hatua ya kuendelea kuboresha mawasiliano baina yetu na jamii tunayoihudumia.

Kupitia Jarida hili, ninyi wadau wetu mtaweza kupata habari na taarifa zetu mbalimbali kwa wakati, pindi tu linapotoka, mwanzoni mwa kila mwezi. Aidha, ili kuwafikieni kwa wingi, Jarida litakuwa la mitandaoni. Mtaweza kulisoma Jarida hili mahala popote mlipo, tena bure kabisa, pasipo kutozwa malipo yoyote.

Ni matumaini yangu kuwa Jarida hili litakidhi malengo yanayotarajiwa katika kuelimisha na kuhabarisha umma. Nawatakia usomaji mwema wa Toleo hili la kwanza na mengine yote yatakayofuata.

Asanteni na karibuni!

## HABARIKA NA KUELIMIKA KUPITIA SAUTI YA TSC

Wapendwa wadau wetu, tunawakaribisha kusoma Jarida hili la Mtandaoni, lenye kulenga kuhabarisha na kuelimisha umma kuhusu kazi mbalimbali zinazofanywa na Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC).

Sisi TSC, tukiwa ni mojawapo ya Taasisi za Serikali, tuna jukumu la kuhakikisha umma unapata taarifa sahihi zinazohusu sekta yetu. Ni kwa sababu hiyo, tumeamua kuongeza hii nyenzo nyingine ya mawasiliano, ambayo tunaamini itapanua zaidi wigo wa wananchi kupata habari na taarifa zetu mbalimbali.

Jarida hili linaandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini na litakuwa likitoka mwanzoni mwa kila mwezi. Litasambazwa katika mitandao mbalimbali ya kijamii. Pia litakuwa likipatikana katika Tovuti ya TSC (www.tsc.go.tz).

Wataalamu wetu wametumia aina tofauti tofauti za uandishi ili kumfanya msomaji asichoke kulisoma Jarida husika. Ndani ya Jarida, Msomaji atakutana na habari fupi, makala, matukio katika picha na katuni.

Tunakaribisha maoni mbalimbali na ushauri. Fika Kitengo cha Mawasiliano Serikalini cha Tume au wasiliana nasi kwa anuani ifuatayo:

**Mhariri Mkuu**
**SAUTI YA TSC**
**Tume ya Utumishi wa Walimu**
**Mtaa wa Mtendeni, S.L.P 353, DODOMA.**

**Simu: 0739-669610 & 0735-255238**
**Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz**

## BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti**
**Moses Chitama**


**Wajumbe**
Richard Odongo
Revocatus Misonge
Mectildis Kapinga
Lameck Mbeya

**Mhariri Mkuu**
Veronica Simba

**Mhariri Msaidizi**
Adili Mhina

**Msanifu Kurasa**
Lucas Gordon

## KATUNI



# NAIBU WAZIRI SILINDE AAGIZA TSC IPEWE OFISI ZENYE HADHI




*Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde (wa tatu - kulia), akiungana na Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kuimba wimbo maarufu wa 'Solidarity Forever'. Naibu Waziri alifungua Mkutano huo mjini Morogoro, Januari 25, 2021. Kushoto kwake ni Mwenyekiti wa TSC, Profesa Willy Komba na kulia kwake ni Kaimu Katibu wa TSC, Moses Chitama.*

Aidha, aliitaka Tume kuhakikisha inawawezesha Walimu kujitambua na kuelewa sheria, kanuni, taratibu, haki na wajibu wao.

Vilevile, aliipongeza Tume kwa kutekeleza majukumu yake kwa weledi na kwa moyo wa uzalendo, pamoja na changamoto mbalimbali zinazowakabili. Pamoja na kutoa pongezi, aliitaka Tume kuendelea kutoa huduma bora kwa Walimu.

"Sote tunafahamu kuwa tunapotoa huduma bora kwa Mwalimu inamwezesha kutekeleza majukumu yake shuleni kwa ufanisi hatimaye kuinua kiwango cha elimu nchini."

Naibu Waziri aliihakikishia Tume kuwa ushirikiano uliopo katika utendaji kazi kati ya Tume na Ofisi ya Rais – TAMISEMI ni endelevu. Aidha, aliongeza kuwa Ofisi yake itaendelea kusisitiza kila Wilaya kuhakikisha kazi za kushughulikia masuala ya kiutumishi ya Walimu zinatekelezwa kwa ushirikiano ili kuleta tija na ufanisi katika suala zima la kuwahudumia walimu.

Awali, akiwasilisha hotuba ya kumkaribisha Mgeni Rasmi, Mwenyekiti wa Tume, Profesa Willy Komba alibainisha changamoto kadhaa zinazoikabili, ikiwa ni pamoja na kutokuwa na jengo la Ofisi za Tume Makao Makuu na Wilaya.



*Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), wakimsikiliza Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) David Silinde (hayupo pichani) wakati akifungua Mkutano huo mjini Morogoro, Januari 25, 2021.*

# NAIBU WAZIRI SILINDE AAGIZA TSC IPEWE OFISI ZENYE HADHI



*Kaimu Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Moses Chitama akizungumza wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Tume hiyo, uliofanyika Jaunuari 25, 2021 mjini Morogoro. Katikati ni Mgeni Rasmi ambaye ni Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde na kulia ni Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Profesa Willy Komba.*



*Mjumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Abihudi Hemba akitoa neno la shukrani kwa niaba ya Baraza hilo kwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) David Silinde (hayupo pichani) baada ya kufungua Mkutano huo mjini Morogoro, Januari 25, 2021.*

Alisema changamoto nyingine ni baadhi ya waajiri kutokuzingatia sheria, kanuni na taratibu katika kushughulikia masuala ya kinidhamu ya Walimu.

"Mfano kuchelewa kuwasilisha mashtaka kwa Mamlaka ya Nidhamu, kuchukua jukumu la kutoa adhabu kinyume cha utaratibu na kuwaondoa Walimu kwenye mfumo wa malipo kabla ya mchakato wa mashauri kuanza na kukamilika," amefafanua Profesa Komba.



*Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) David Silinde (katikati-waliokaa), akiwa katika picha ya pamoja na Menejimenti ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), muda mfupi baada ya kufungua Mkutano wa Baraza la Wafanyakzi wa Tume hiyo Januari 25, 2021 mjini Morogoro. Kushoto kwa Naibu Waziri ni Mwenyekiti wa TSC, Profesa Willy Komba na kulia kwake ni Kaimu Katibu wa TSC, Moses Chitama.*

Mkutano huo wa siku mbili ulihudhuriwa pia na Kaimu Katibu wa Tume, Moses Chitama, Menejimenti ya Tume pamoja na wawakilishi mbalimbali kutoka wilaya zote nchini.

Tume ya Utumishi wa Walimu ni Mamlaka ya Ajira na Nidhamu kwa Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari za Serikali, Tanzania Bara. Naibu Waziri David Silinde ndiye amepewa wajibu wa kusimamia Taasisi hii pamoja na nyingine zilizo chini ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

# Kamati za TSC zatakiwa kutenda haki kwa Walimu

**Na Adili Mhina**

Wajumbe wa Kamati za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ngazi ya Wilaya, wametakiwa kuzingatia maadili na miiko ya utumishi katika kutekeleza majukumu yao, ili waweze kufikia malengo ya Tume ya kutoa huduma bora na kwa haki kwa walimu wote nchini.

Kauli hiyo ilitolewa Februari 8, 2021 na Mwenyekiti wa TSC, Profesa Willy Komba wakati akifungua mafunzo yaliyowahusisha Wajumbe wa Kamati za TSC kutoka Wilaya za Mikoa ya Pwani, Dar es Salaam na Morogoro yaliyofanyika mjini Morogoro.

Alieleza kuwa kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Na. 25 ya mwaka 2015 na Kanuni zake za mwaka 2016, Kamati za Wilaya zimepewa mamlaka ya kusimamia Maadili na Maendeleo ya walimu, hivyo mamlaka hayo yakitumika vibaya haki haiwezi kutendeka kwa walimu.

"Kamati za Wilaya zimepewa nguvu kubwa kisheria katika kuamua masuala ya ajira, maadili na maendeleo ya walimu, hivyo kitu kikubwa mnachopaswa kuzingatia ni maadili ya utumishi



*Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Profesa Willy Komba akitoa hotuba ya ufunguzi wa mafunzo ya Kamati za TSC ngazi ya Wilaya, yaliyofanyika mkoani Morogoro, Februari 8, 2021.*



*Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Profesa Willy Komba (katikati - waliokaa), akiwa katika picha ya pamoja na Makamishna wa Tume (waliokaa) pamoja na baadhi ya wajumbe wa mafunzo ya Kamati za Wilaya, yaliyofanyika mkoani Morogoro, Februari 8, 2021. Kushoto kwa Mwenyekiti ni Kaimu Katibu wa Tume, Moses Chitama na wa kwanza kulia (aliyekaa) ni Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu, Robert Lwikolela.*



*Kaimu Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Moses Chitama akitoa maelezo kwa wajumbe wa Kamati za Wilaya (hawapo pichani), katika mafunzo ya Kamati hizo yaliyofanyika mkoani Morogoro, Februari 8, 2021.*

# Kamati za TSC zatakiwa kutenda haki kwa Walimu



*Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Robert Lwikolela akitoa mada juu ya Nguzo za Maadili ya Kazi ya Ualimu wakati wa Mafunzo ya Kamati za TSC ngazi ya Wilaya, mkoani Morogoro, Februari 8, 2021.*

wenu ili muweze kutenda haki kwa walimu kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zinazohusika," alisema.

Profesa Komba alieleza kuwa Tume imebaini changamoto kadhaa za kiutendaji katika Kamati za Wilaya, jambo linalosababisha baadhi ya walimu kunyimwa haki zao za msingi hususan wakati wa kushughulikia mashauri yao ya nidhamu.

"Tukiwa tunashughulikia rufaa za walimu, tumeona kuwa miongoni mwa hoja nyingi za



*Baadhi ya wajumbe wa mafunzo ya Kamati za Wilaya za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), wakifuatilia mada zilizokuwa zikiwasilishwa katika mafunzo hayo, yaliyofanyika Februari 8, 2021 mkoani Morogoro. Mafunzo hayo yalihusisha Kamati za TSC kutoka Wilaya za Mikoa ya Pwani, Dar es Salaam na Morogoro.*

warufani ni Mamlaka za Nidhamu (Kamati za Wilaya) kutozingatia taratibu za uendeshaji wa mashauri zilizowekwa kwa mujibu wa sharia, kitu ambacho tumeona kinakwamisha malengo ya Tume katika kutoa huduma bora kwa walimu," alisema Profesa Komba.

Alisema kuwa baada ya kubaini changamoto hiyo, Tume imeanza kuwajengea uwezo wajumbe wa Kamati za Wilaya ili wawe na uelewa wa kutosha wa sheria, kanuni na taratibu za utendaji wao na kuhakikisha kuwa kila mwalimu anahudumiwa kwa haki na kwa wakati.

Hata hivyo, Mwenyekiti alizitahadharisha Kamati hizo kuwa suala la uelewa wa sheria ni jambo moja na utekelezaji wa sheria ni jambo jingine.

Alifafanua kuwa, wajumbe

# Kamati za TSC zatakiwa kutenda haki kwa Walimu

wasipokuwa waadilifu wanaweza kukiuka taratibu makusudi ili kutimiza matakwa yao bila kujali maumivu ya walimu yanayosababishwa na kunyimwa haki zao.

"Tunawapa mafunzo kwa sababu ni wajibu wa Tume kuwajengea uwezo ili muweze kutekeleza majukumu yenu kwa kuzingatia sheria. Hata hivyo, mnaweza kuwa na uelewa wa kutosha lakini msipokuwa waadilifu bado hamtawatendea haki walimu. Ninawasihi, kila mmoja azingatie maadili ya kazi yake ili Serikali iweze kufikia azma yake ya kuwahudumia walimu kwa haki," alisema.

Naye Kaimu Katibu wa TSC, Moses Chitama alieleza kuwa Kamati za Wilaya zina wajibu wa kuwaelimisha walimu kuhusu haki na wajibu wa kazi yao na siyo kukaa na kusubiri walimu wakosee ili wawachukulie hatua za kinidhamu.

Aliongeza kuwa lengo kubwa la kuanzishwa kwa TSC ni kurahisisha huduma kwa walimu ili waweze kufundisha wanafunzi kwa ufanisi. Hivyo, ni wajibu wa kila mjumbe kuelewa kuwa Tume ina wajibu wa kuwalea walimu ili wasijiingize katika ukiukaji wa maadili na hivyo kuadhibiwa.

"Ninapenda tuwe na uelewa wa pamoja kuwa Tume haipo kwa ajili ya kuwafukuza walimu tu. Wapo wajumbe wa Kamati tangu wanachaguliwa hadi wanamaliza muda wao, hawajawahi kuwatembelea walimu na kuwaelimisha kuhusu wajibu na haki zao. Ni jambo baya sana endapo huko wilayani unakaa tu kusubiri uletewe shauri la mwalimu ili umfukuze kazi," alisema Chitama.

Kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu, Kamati za Wilaya ni Mamlaka ya Nidhamu kwa walimu na miongoni mwa majukumu yao ni kushughulikia masuala ya ajira na maendeleo ya walimu ikiwemo kumpandisha cheo/daraja mwalimu, kumbadilishia muundo wa kazi mwalimu aliyejiendeleza kimasomo pamoja na masuala ya kusimamia nidhamu na maadili ya walimu.

Mafunzo hayo yalihudhuriwa pia na wajumbe wa Tume ya Utumishi wa Walimu ambao pamoja na majukumu mengine kwa mujibu wa sheria, wamepewa mamlaka ya kuamua rufaa za walimu wanaopinga uamuzi uliotolewa na Kamati za Wilaya.



*Baadhi ya wajumbe wa mafunzo ya Kamati za Wilaya za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), wakifuatilia mada zilizokuwa zikiwasilishwa katika mafunzo hayo, yaliyofanyika Februari 8, 2021 mkoani Morogoro. Mafunzo hayo yalihusisha Kamati za TSC kutoka Wilaya za Mikoa ya Pwani, Dar es Salaam na Morogoro.*

# WALIMU WAHAMASISHWA KUJIENDELEZA KIELIMU

**Na Veronica Simba**

Serikali imewahamasisha Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari nchini, kujiendeleza kielimu katika ngazi mbalimbali ili kuboresha zaidi utendaji wao wa kazi.

Wito huo ulitolewa jijini Dodoma, Januari 7, 2021 na Kaimu Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Moses Chitama wakati akizungumza na Wajumbe wa Mkutano wa Pili wa Umoja wa Walimu Wakuu wa Shule za Msingi Tanzania Bara.

Akifafanua, alisema kuwa, kujiendeleza kielimu ni haki ya msingi kwa watumishi wote wa umma wakiwemo walimu, ndiyo maana Serikali kupitia Tume imekuwa ikiwahamasisha kuitumia fursa hiyo ipasavyo.




*Kaimu Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Moses Chitama (katikati), akifafanua masuala mbalimbali kuhusu wajibu na haki za Walimu, katika mkutano wa pili wa Umoja wa Walimu Wakuu wa Shule za Msingi Tanzania Bara (hawapo pichani), Dodoma, Januari 7, 2021.*



*Kaimu Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Moses Chitama (Meza Kuu), akifafanua masuala mbalimbali kuhusu wajibu na haki za Walimu, katika mkutano wa pili wa Umoja wa Walimu Wakuu wa Shule za Msingi Tanzania Bara, Dodoma, Januari 7, 2021.*

“

**Tumekuwa tukipata rufaa nyingi za kesi za Walimu ambao walitoroka kazini na kwenda masomoni hivyo kufukuzwa kazi. Serikali inapenda walimu msome lakini fuateni taratibu zilizowekwa.”**

# WALIMU WAHAMASISHWA KUJIENDELEZA KIELIMU

Chitama alikemea tabia ya baadhi ya Walimu Wakuu wa Shule za Msingi na Wakuu wa Shule za Sekondari Tanzania Bara, ambao hukataa kutoa ruhusa kwa watumishi walio chini yao wenye nia ya kujiendeleza kielimu.

Hata hivyo, Kaimu Katibu huyo alisisitiza kuwa Walimu wote wa shule za umma wenye nia ya kujiendeleza kielimu, wanapaswa kuzingatia taratibu zilizowekwa na Mamlaka ikiwemo kufuata Mpango wa Mafunzo.

Aidha, aliwasisitiza kuhakikisha wanapata ruhusa ya maandishi kutoka kwa Wakuu wao, kabla ya kwenda masomoni kwani kinyume chake



*Mkurugenzi Msaidizi wa Ajira na Maendeleo ya Walimu kutoka Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mectildis Kapinga, akizungumzia kuhusu upandaji madaraja kwa walimu, wakati wa mkutano wa pili wa Umoja wa Walimu Wakuu wa Shule za Msingi Tanzania Bara (hawapo pichani), uliofanyika jijini Dodoma, Januari 7, 2021.*



*Mkurugenzi Msaidizi wa Ajira na Maendeleo ya Walimu kutoka Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mectildis Kapinga (katikati), akifafanua jambo kwa Mwalimu Huruma Muya kutoka Kigamboni Dar es Salaam (kushoto) na Mwalimu Simon Mwemutsi kutoka Ifakara Morogoro (kulia), muda mfupi baada ya kuwasilisha mada kuhusu haki na wajibu kwa walimu katika mkutano wa pili wa Umoja wa Walimu Wakuu wa Shule za Msingi Tanzania Bara (hawapo pichani), Januari 7, 2021 jijini Dodoma.*



*Kaimu Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Moses Chitama (kulia) akifafanua jambo kwa Mwalimu Raymond Lyoba kutoka Urambo, Tabora, muda mfupi baada ya kuwasilisha mada kuhusu haki na wajibu kwa walimu katika mkutano wa pili wa Umoja wa Walimu Wakuu wa Shule za Msingi Tanzania Bara (hawapo pichani), Januari 7, 2021 jijini Dodoma.*

# WALIMU WAHAMASISHWA KUJIENDELEZA KIELIMU

watakabiliwa na mashtaka ya utoro kazini ambayo adhabu yake ni kufukuzwa kazi.

"Tumekuwa tukipata rufaa nyingi za kesi za Walimu ambao walitoroka kazini na kwenda masomoni hivyo kufukuzwa kazi. Serikali inapenda walimu msome lakini fuateni taratibu zilizowekwa," alisisitiza.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Msaidizi wa Ajira na Maendeleo ya Walimu kutoka TSC, Mectildis Kapinga, akifafanua kuhusu utaratibu wa kupanda vyeo, alieleza Mkutano huo kuwa, kanuni inaelekeza kutompandisha cheo mtumishi yeyote wa umma akiwa masomoni, hadi pale anapohitimu ndipo mchakato wa kumpandisha hufanyiwa kazi.



*Kaimu Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Moses Chitama (wa tatu-kushoto) na Mkurugenzi Msaidizi wa Ajira na Maendeleo ya Walimu wa Tume, Mectildis Kapinga (wa tatu-kulia), wakiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya wajumbe wa mkutano wa pili wa Umoja wa Walimu Wakuu wa Shule za Msingi Tanzania Bara, muda mfupi baada ya kuwasilisha mada kuhusu haki na wajibu kwa walimu, Januari 7, 2021 jijini Dodoma.*

"Naomba mtambue kuwa utaratibu huo ni kwa watumishi wote wa umma, na siyo kwa walimu pekee kama ambavyo baadhi yenu mmekuwa mkinung'unika," alifafanua Kapinga.

Mkutano huo wa siku tatu, ulianza Januari 5, 2021 huku ukiongozwa na kaulimbiu isemayo uongozi na usimamizi makini wa elimu, utaimarisha Tanzania katika uchumi wa kati.

Tume ya Utumishi wa Walimu ni Mamlaka ya Ajira na Nidhamu kwa walimu wa shule za msingi na sekondari Tanzania Bara, walio kwenye utumishi wa umma.






*Sehemu ya wajumbe wa mkutano wa pili wa Umoja wa Walimu Wakuu wa Shule za Msingi Tanzania Bara, wakifuatilia mkutano huo uliofanyika jijini Dodoma, Januari 7, 2021.*

# Ijue Tume ya Utumishi wa Walimu

**Na Adili Mhina**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ni Mamlaka ya Ajira na Nidhamu kwa Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari walio kwenye Utumishi wa Umma, Tanzania Bara. Tume hii imeundwa kwa Sheria Namba 25 ya mwaka 2015 na ilianza kutekeleza majukumu yake Aprili 1, 2016.

Hii ina maana kuwa Walimu wengine (wasio katika Utumishi wa Umma) hawashughulikiwi chini ya Sheria hii, hao wanashughulikiwa na Waajiri wao, chini ya Sheria ya Utumishi wa Umma Namba 8 ya Mwaka 2002 na Sheria ya Marekebisho Namba 18 ya Mwaka 2007.

Ili kuielewa vyema TSC, ni vyema ni vyema kufahamu historia ya usimamizi wa masuala ya utumishi wa walimu katika nchi yetu ambayo yamepita katika hatua mbalimbali tangu tupate uhuru.

Mara baada ya uhuru, Tanzania wakati huo ikiitwa Tanganyika, Serikali iliamua kuunganisha utumishi wa walimu wote wa Serikali na wa sekta binafsi chini ya Sheria Namba 6 ya mwaka 1962 ya Huduma kwa Walimu (Unified Teaching Service – UTS).

UTS ilishughulikia utumishi wa walimu wote wa Serikali na Waajiri wengine katika masuala yaliyohusu ajira, kuthibitishwa kazini, kupandishwa cheo, maadili na nidhamu. Mwalimu aliyeajiriwa na Mwajiri mwingine nje ya Serikali, alijaza mkataba na Mwajiri wake na kuuwasilisha UTS kwa ajili ya kusajiliwa na kupewa namba ya usajili. Mapendekezo ya kuthibitishwa kazini na kupandishwa cheo yaliwasilishwa UTS, na Waajiri wote walitekeleza uamuzi uliotolewa na UTS.

Kadri walimu walivyokuwa wakiongezeka, suala la usimamizi wa utumishi wao lilikuwa na changamoto ambapo matatizo ya walimu kukosa huduma yalianza kujitokeza.

Mwaka 1980 – 1982, Tume ya Rais ya Elimu chini ya Mheshimiwa Jackson Makweta ilibaini kwamba muundo wa UTS ambayo ilikuwa kitengo kidogo kwenye iliyokuwa Wizara ya Elimu na Utamaduni na Ofisi za Wakurugenzi wa Maendeleo wa Mikoa na Wilaya usingeweza kukabiliana na ongezeko kubwa la walimu.

Kutokana na changamoto hizo, Mwaka 1989 ilianzishwa Tume ya Utumishi wa Walimu (Teachers' Service Commission -TSC) ambayo ilikuwa ni Idara inayojitegemea chini ya Wizara ya Elimu na Utamaduni. Majukumu



*Walimu Wakuu na Wakuu wa Shule wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, wakiwa katika hali ya furaha, wakati wa mkutano wao na viongozi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (hawapo pichani) uliofanyika jijini Dodoma.*

> **"Lengo la kuanzishwa kwa TSC ni kuongeza ufanisi katika kuwahudumia Walimu ambao ni kundi linalochukua zaidi ya asilimia hamsini (50%) ya watumishi wa umma."**

# Ijue Tume ya Utumishi wa Walimu



*Aliyekuwa Mkurugenzi wa Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Christina Hape akitoa maelezo kuhusu masuala mbalimbali ya TSC kwa wanafunzi waliotembelea Banda la Tume, wakati wa Maonesho ya Nane Nane, mkoani Simiyu, Agosti 2020.*

yote yaliyokuwa yakitekelezwa na UTS yalihamishiwa TSC.

Kufuatia Sera ya Ajira na Menejimenti katika Utumishi wa Umma ya mwaka 1999, Utumishi wa Umma uliunganishwa. Sheria ya Utumishi wa Umma Namba 8 ya mwaka 2002 ilianzishwa na kufuta iliyokuwa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Namba 1 ya mwaka 1989. TSC ilifanywa kuwa Idara ya Tume ya Utumishi wa Umma (PSC), iliyojulikana kama Idara ya Utumishi wa Walimu (TSD).

Hata hivyo, Serikali iliona kuwa TSD haiwezi kufikia malengo tarajiwa ikiwa chini ya PSC. Hivyo, mwaka 2015 Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilitunga Sheria Namba 25 iliyoanzisha Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ambayo ndiyo inayosimamia utumishi wa walimu kwa sasa.

Lengo la kuanzishwa kwa TSC ni kuongeza ufanisi katika kuwahudumia Walimu ambao ni kundi linalochukua zaidi ya asilimia hamsini (50%) ya watumishi wa umma.

Tume ya Utumishi wa Walimu inaundwa na Mwenyekiti ambaye huteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wajumbe wengine 8 ambao huteuliwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Mtendaji Mkuu wa Tume ni Katibu ambaye huteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

TSC inatekeleza majukumu yake kupitia ofisi 140 ambapo ofisi 139 zipo katika kila Wilaya kwa Tanzania bara na ofisi moja ni ya Makao Makuu ya Tume ambayo ipo jijini Dodoma.

Kwa mujibu wa Sheria Namba 25 ya mwaka 2015, TSC ina majukumu mbalimbali

# Ijue Tume ya Utumishi wa Walimu

ikiwemo kushughulikia masuala ya ajira na maendeleo ya walimu, kushughulikia mafao ya wastaafu na mirathi ambayo hayashughulikiwi na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, kwa kukokotoa mafao na kuwasilisha kwa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Hazina kwa malipo pamoja na kusimamia maadili na nidhamu kwa walimu.

Majukumu mengine ni pamoja na kufanya tafiti kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu utumishi wa walimu, kuhakikisha uwiano sawa katika upangaji wa walimu ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na Shule na kusimamia programu za mafunzo ya walimu kazini.

TSC pia ina jukumu la kuandaa kanzidata, takwimu na taarifa za utekelezaji za robo mwaka na mwaka, kufanya tathmini ya hali ya walimu na kumshauri Waziri anayehusika na mafunzo ya walimu kuhusu idadi, aina ya mafunzo na uhitaji wa walimu nchini.

Dira ya Tume ni kuwa Taasisi inayoongoza katika kutoa huduma bora kwa Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari walio kwenye Utumishi wa Umma na dhamira yake ni kutoa huduma bora na kwa wakati kwa Walimu husika kwa kusimamia masuala ya ajira na nidhamu ili kukuza kiwango cha elimu.

Kwa ufupi tunaweza kusema TSC inashughulika na walimu katika maeneo makubwa mawili ambayo ni eneo la Ajira na Maendeleo pamoja na eneo la Maadili na Nidhamu.

Katika suala la Ajira na Maendeleo ya Walimu, Tume inashughulika na kumsajili mwalimu pale anapoajiriwa, kumthibitisha kazini, kumpandisha cheo, kumbadilishia kazi/cheo mwalimu aliyejiendeleza kielimu, kutoa vibali vya kustaafu pamoja na mafao ya hitimisho la kazi ya walimu yanayolipwa na hazina.

Kwa upande wa Nidhamu, Wakuu wa Shule ndiyo mamlaka ya kwanza ya nidhamu ya walimu katika ngazi ya shule ambao mamlaka yao katika kushughulikia nidhamu kwa walimu yameainishwa katika kifungu cha 12 (3) cha Kanuni za Tume ya Utumishi wa Walimu za mwaka 2016.

Kamati ya Tume ya Utumishi wa Walimu ngazi ya Wilaya, ndiyo mamlaka ya rufaa kwa walimu ambao hawakuridhika na uamuzi uliotolewa na Mkuu wa Shule. Pia, ni mamlaka ya nidhamu ya walimu kwa makosa yaliyoainishwa katika kifungu cha 12 (2) cha Kanuni za Tume ya Utumishi wa Walimu za mwaka 2016.

**“Endapo kuna upande ambao hautaridhika na maamuzi ya Kamati ya Tume ngazi ya Wilaya, unaweza kukata rufaa kwa Tume Makao Makuu, ndani ya siku 45 tangu kupokea uamuzi wa shauri husika.”**

Endapo kuna upande ambao hautaridhika na maamuzi ya Kamati ya Tume ngazi ya Wilaya, unaweza kukata rufaa kwa Tume Makao Makuu, ndani ya siku 45 tangu kupokea uamuzi wa shauri husika.

Aidha, endapo Mrufani hataridhishwa na uamuzi wa Tume Makao Makuu, anayo haki ya kukata rufaa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ndani ya siku 45 tangu siku ya kupokea uamuzi wa rufaa yake.

Serikali kupitia TSC imedhamiria kuwasaidia walimu kwa kuhakikisha wanakuwa na uelewa wa kutosha juu ya wajibu na haki zao, kutatua kero na malalamiko yao, kuongeza morali ya utendaji wa kazi na kuhakikisha walimu wanapata haki zao kwa wakati.

Hivyo, ili kutoa huduma bora na kwa wakati, wadau wote wanapaswa kuwa na mahusiano na ushirikiano wa karibu ili kuwaondolea walimu usumbufu pale wanapohitaji huduma.

Waajiri wote wanahimizwa kuendelea kutoa ushirikiano wa karibu kwa Tume ngazi ya Wilaya, ili kuendea kuboresha masuala ya Utumishi wa Walimu nchini. Vilevile, Walimu wanapaswa kuzingatia Miiko na Maadili ya kazi ili kujiepusha na makosa yanayoweza kuathiri utumishi wao.

# TSC YAWAAGA WASTAAFU WAKE

**Nawasisitiza muendelee kufanya kazi kwa weledi ili tufikie malengo na kuwa Taasisi ya mfano wa kuigwa kwa kuihudumia vyema kada ya walimu na hivyo kuwezesha kuinua zaidi kiwango cha elimu nchini."**

**Na Veronica Simba**



*Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Profesa Willy Komba, akitoa hotuba ya kufunga Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Tume, mjini Morogoro, Januari 26, 2021. Kushoto ni Kaimu Katibu wa TSC, Moses Chitama.*

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imewaaga rasmi watumishi wake 10 waliostaafu na wale wanaotarajiwa kustaafu hivi karibuni, akiwemo aliyekuwa Katibu wa Tume, Winifrida Rutaindurwa.

Tukio hilo lilifanyika Januari 26, 2021 mjini Morogoro, wakati wa kuhitimisha Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi uliohudhuriwa na Mwenyekiti wa Tume, Profesa Willy Komba, Kaimu Katibu wa Tume, Moses Chitama, Menejimenti na wawakilishi kutoka wilaya zote za Tanzania Bara.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo fupi, Profesa Komba aliwapongeza wastaafu hao kwa utumishi uliotukuka na kuwaomba waendelee kuwa Mabalozi wa Tume kokote watakakokwenda.

Kwa upande wake, Katibu Mstaafu wa Tume, Bibi Rutaindurwa, akizungumza kwa niaba ya wastaafu wenzake, alishukuru ushirikiano walioupata kutoka kwa watumishi wote na kuwaasa kuendeleza mshikamano baina




*Katibu Mstaafu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Winifrida Rutaindurwa (kulia), akipokea zawadi kutoka kwa Mwenyekiti wa TSC, Profesa Willy Komba, wakati wa hafla fupi ya kuwaaga wastaafu wa Tume, iliyofanyika Januari 26, 2021, mjini Morogoro. Wa kwanza kushoto ni Kaimu Katibu wa TSC, Moses Chitama.*

# TSC YAWAAGA WASTAAFU WAKE

yao.

Akitoa hotuba ya kufunga Mkutano huo wa Baraza la Wafanyakazi, Profesa Komba alibainisha kuwa umekuwa wenye mafanikio makubwa huku akiwakumbusha wajumbe kuzingatia maadili ya kazi na weledi ili kuiwezesha Tume kufikia malengo yaliyowekwa na Serikali.

"Nawasisitiza muendelee kufanya kazi kwa weledi ili tufikie malengo na kuwa Taasisi ya mfano wa kuigwa kwa kuihudumia vyema kada ya walimu na hivyo kuwezesha kuinua zaidi kiwango cha elimu nchini."

Aidha, alitumia fursa hiyo kuwakumbusha kuwa Serikali ya Awamu ya Tano imedhamiria kuondoa uzembe na vitendo vya rushwa mahali pa kazi pamoja na kubana matumizi yasiyo ya lazima, hivyo akawataka kujiepusha na vitendo hivyo badala yake kila mmoja atimize wajibu wake ipasavyo.



*Katibu Mstaafu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Winifrida Rutaindurwa, akizungumza na Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa Tume hiyo, wakati wa hafla fupi ya kuwaaga wastaafu iliyofanyika Januari 26, 2021 mjini Morogoro.*



*Baadhi ya watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), waliostaafu na wanaotarajiwa kustaafu hivi karibuni, wakiungana na Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa Tume, kuimba kwa furaha wakati wa hafla fupi ya kuwaaga wastaafu hao iliyofanyika Januari 26, 2021 mjini Morogoro.*

Wastaafu wengine walioagwa ni pamoja na Christina Hape aliyekuwa Makao Makuu Dodoma, Corona Maira (Ilemela), Anna Mutungi (Bukoba), Fanuel Edward (Musoma), Rahim Mgongo (Lushoto) na Vicent Shemsanga (Kibaha).

Wengine ni Matilda Philemon (Kigoma), Elineema Mtaita (Morogoro) na Magdalena Nakitundu (Tabora).

Mkutano huo wa siku mbili wa Baraza la Wafanyakazi wa Tume ya Utumishi wa Walimu, ulifunguliwa na Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde.

# TSC YAWAAGA WASTAAFU WAKE













*Watumishi mbalimbali wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) waliostaafu na wanaotarajiwa kustaafu hivi karibuni, wakipokea zawadi kutoka kwa Mwenyekiti wa Tume, Profesa Willy Komba, wakati wa hafla fupi ya kuwaaga iliyofanyika mjini Morogoro, Januari 26, 2021.*

# MATUKIO MBALIMBALI WAKATI WA HAFLA YA KUWAAGA WASTAAFU WA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC) ILIYOFANYIKA JANUARI 26, 2021 MKOANI MOROGORO













# MATUKIO MBALIMBALI WAKATI WA HAFLA YA KUWAAGA WASTAAFU WA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC) ILIYOFANYIKA JANUARI 26, 2021 MKOANI MOROGORO













# MATUKIO MBALIMBALI WAKATI WA MKUTANO WA BARAZA LA WAFANYAKAZI WA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC) ULIOFANYIKA JANUARI 25 NA 26, 2021 MKOANI MOROGORO













# MATUKIO MBALIMBALI WAKATI WA MKUTANO WA BARAZA LA WAFANYAKAZI WA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC) ULIOFANYIKA JANUARI 25 NA 26, 2021 MKOANI MOROGORO














# MATUKIO MBALIMBALI WAKATI WA MKUTANO WA BARAZA LA WAFANYAKAZI WA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC) ULIOFANYIKA JANUARI 25 NA 26, 2021 MKOANI MOROGORO















# MATUKIO MBALIMBALI WAKATI WA MKUTANO WA BARAZA LA WAFANYAKAZI WA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC) ULIOFANYIKA JANUARI 25 NA 26, 2021 MKOANI MOROGORO













# HATUWAADHIBU WALIMU ILI KUWAKOMOA BALI KUWAJENGA KIMAADILI - CHITAMA



*Kaimu Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Moses Chitama.*

**Ndiyo maana walimu hufundishwa tangu wakiwa vyuoni namna bora ya kuwalea watoto watakaokwenda kuwafundisha ili wawe raia wema katika jamii na Taifa kwa ujumla."**

**Na Veronica Simba**

Kaimu Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania (TSC), Moses Chitama ameitaka jamii kuelewa kwamba adhabu zinazotolewa kwa walimu wanaobainika kwenda kinyume na maadili hazilengi kuwakomoa bali zipo kisheria ili kuhakikisha nidhamu na maadili ya kada hiyo yanazingatiwa.

Aliyasema hayo kwa nyakati tofauti hivi karibuni wakati akizungumza na vyombo mbalimbali vya habari nchini kuhusu nidhamu na maadili kwa walimu nchini.

Chitama alieleza kuwa, ualimu ni taaluma kama zilivyo taaluma nyingine hivyo ina miiko, taratibu na sheria zake zinazoiongoza na zinapokiukwa, Tume inawajibika kuchukua hatua ili kuhakikisha shule zinabaki kuwa mahala salama na sahihi kwa watoto wanaohusika.

"Ndiyo maana walimu hufundishwa tangu wakiwa vyuoni namna bora ya kuwalea watoto watakaokwenda

# HATUWAADHIBU WALIMU ILI KUWAKOMOA BALI KUWAJENGA KIMAADILI - CHITAMA

**Sasa kweli kwa hali kama hiyo ambapo wanafunzi wanakoseshwa haki yao ya msingi ya masomo na wengine kunyanyaswa kijinsia, unatarajia Tume ikae kimya tu? Ni lazima tuchukue hatua stahiki ili kukomesha hali hiyo."**

kuwafundisha ili wawe raia wema katika jamii na Taifa kwa ujumla."

Akizungumzia ukiukwaji wa maadili unaofanywa na baadhi ya walimu, Chitama alikiri kuwa tatizo hilo lipo na kuongeza kuwa changamoto ambayo imekithiri kwa sasa ni baadhi ya walimu kujihusisha kimapenzi na wanafunzi.

Alisema, Tume ya Utumishi wa Walimu, ambayo ni Mamlaka ya Nidhamu, imekuwa ikilikemea sana suala hilo na imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali inayolenga kulitatua ikiwemo kutoa semina za kuwajengea uelewa walimu na kwa wanaothibitika kutenda kosa hilo, hupewa adhabu ya kufukuzwa kazi.

Aidha, alitaja changamoto nyingine kuwa ni utoro kazini kwa baadhi ya walimu ambapo alibainisha kuwa uchunguzi uliofanywa na Tume umebaini kuwa baadhi ya wanaotoroka huenda kufanya kazi katika shule za binafsi huku wakiendelea kupokea mshahara wa serikali.

"Sasa kweli kwa hali kama hiyo ambapo wanafunzi wanakoseshwa haki yao ya msingi ya masomo na wengine kunyanyaswa kijinsia, unatarajia Tume ikae kimya tu? Ni lazima tuchukue hatua stahiki ili kukomesha hali hiyo," alisisitiza Chitama.

Kwa upande mwingine, Kaimu Katibu huyo amewaasa wazazi kutimiza wajibu wao kwa kushirikiana na walimu katika malezi ya watoto badala ya kuwaachia walimu peke yao jukumu hilo.

Akifafanua, alisema baadhi ya wazazi wamekuwa wakikwepa kutimiza wajibu wao wa malezi kwa watoto kwa kisingizio cha kukosa muda kutokana na kazi wanazozifanya kujipatia kipato, hali inayochangia kwa kiasi kikubwa mmomonyoko wa maadili kwa watoto.

Tume ya Utumishi wa Walimu ni Mamlaka ya Ajira na Nidhamu kwa walimu wa shule za msingi na sekondari walio kwenye utumishi wa umma, Tanzania Bara.

Imeundwa kwa Sheria Namba 25 ya mwaka 2015 na ilianza kufanya kazi rasmi mwaka 2016 baada ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitisha sharia na kanuni zake.




*Kaimu Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Moses Chitama.*

# WALIMU WATAJWA KUWA CHANZO KIKUU CHA MAENDELEO YA NCHI

**Na Veronica Simba**

Imeelezwa kuwa walimu ndiyo chanzo kikuu cha maendeleo ya nchi kwakuwa wamepewa dhamana ya kuwalea kiakili na kimwili watoto, ambao wanategemewa na Taifa kuja kuwa viongozi na wataalamu katika nyanja mbalimbali.

Kaimu Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania (TSC), Moses Chitama aliyasema hayo Januari 5 mwaka huu, wakati akiwasilisha mada kuhusu maadili, katika Mkutano wa Pili wa Umoja wa Walimu Wakuu wa Shule za Msingi Tanzania Bara, uliofanyika jijini Dodoma.

Kutokana na dhamana hiyo waliyopewa Walimu, Chitama aliwakumbusha na kuwasisitiza kuwa wanapaswa kutimiza wajibu wao ipasavyo.

Alisema kuwa, TSC ikiwa ni Mamlaka ya Nidhamu kwa



*Kaimu Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Moses Chitama, akiwasilisha mada kuhusu maadili katika mkutano wa pili wa Umoja wa Walimu Wakuu wa Shule za Msingi Tanzania Bara (hawapo pichani), uliofanyika jijini Dodoma, Januari 5, 2021.*

Walimu nchini, imebaini kuwa baadhi ya Walimu wamekuwa hawatimizi wajibu wao ipasavyo katika kuwalea watoto na kwa



*Sehemu ya Wajumbe wa Mkutano wa Pili wa Umoja wa Walimu Wakuu wa Shule za Msingi Tanzania Bara (hawapo pichani), wakifuatilia mada mbalimbali zilizokuwa zikiwasilishwa wakati wa mkutano huo uliofanyika jijini Dodoma, Januari 5, 2021.*

**"Ninyi walimu msiposimamia maadili ya taaluma yenu pamoja na maadili ya watoto mnaowafundisha, tutakuwa na Taifa bovu, lililokosa mwelekeo na lenye mmomonyoko wa maadili."**

# WALIMU WATAJWA KUWA CHANZO KIKUU CHA MAENDELEO YA NCHI

kulitambua hilo, Tume imekuwa ikitumia mbinu mbalimbali katika kuhakikisha suala hilo linatokomezwa ikiwemo kutoa elimu kwa wahusika na kuwachukulia hatua za kinidhamu wanaobainika kutozingatia maadili ya kazi yao.

"Ninyi walimu msiposimamia maadili ya taaluma yenu pamoja na maadili ya watoto mnaowafundisha, tutakuwa na Taifa bovu, lililokosa mwelekeo na lenye mmomonyoko wa maadili.

Akitoa takwimu, Chitama alibainisha kuwa, katika kipindi cha miaka mitano (2016 – 2020), jumla ya walimu 9,819 walifunguliwa mashauri na waajiri wao, ambapo 5,441 kati yao walifukuzwa kazi.

Aidha, alieleza kuwa, katika kipindi hicho, walimu 1,803 walipewa maonyo na makaripio, 520 walipunguziwa mishahara, 244 walisimamishiwa nyongeza ya mishahara na 403 waliteremshwa vyeo.

Kwa upande mwingine, alisema walimu 149 walilipwa fidia na wengine 438 kuachiwa huru.

Akihitimisha, Kaimu Katibu Chitama aliwataka walimu kuwachukulia wanafunzi kama watoto wao wa kuzaa hivyo wawatendee sawa na wanavyotendea familia zao.

Akizungumza katika Mkutano huo, Mkurugenzi kutoka Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), anayesimamia Elimu ya Awali na



*Mkurugenzi Msaidizi kutoka Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), anayesimamia Elimu ya Awali na Msingi, ambaye pia ni Kamishna wa TSC, Susan Nussu, akisisitiza kuhusu maadili ya walimu, wakati wa mkutano wa pili wa Umoja wa Walimu Wakuu wa Shule za Msingi Tanzania Bara (hawapo pichani), uliofanyika jijini Dodoma, Januari 5, 2021.*

Msingi, Susan Nussu, aliwasisitiza walimu kujiepusha na masuala ya udanganyifu wa mitihani katika shule zao.

Alisema wengi hutenda kosa hilo kwa tamaa ya kujitafutia sifa ya ufaulu katika shule zao lakini akawataka kukumbuka kuwa kitendo hicho huwaponza wanafunzi wao kwa kuwasababishia kufutiwa matokeo.

Aidha, aliwataka Walimu Wakuu wa Shule za Msingi kuacha tabia ya kuwapanga walimu wazembe na wavivu kufundisha madarasa ya awali badala yake wawapange walimu wenye weledi ili waweze kuwajengea watoto msingi mzuri wa elimu.

Mkutano huo wa Pili wa Umoja wa Walimu Wakuu wa Shule za Msingi Tanzania, uliongozwa na kaulimbiu isemayo uongozi na usimamizi makini wa elimu, utaimarisha Tanzania katika uchumi wa kati.



JARIDA HILI HUTOLEWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI, **TUME YA UTUMISHI WA WALIMU**

**MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA**
**Simu: +255 (26) 2322402-4** **Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz** **Tovuti: www.tsc.go.tz**

*Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania* *tumeyautumishiwawalimutanzania*